



## USHAURI WA SERA

Shughuli za Nje 2024 - 1

**Sera: Kufunga Maombi ya Ukaguzi wa Hiari wa BRC Kwa Sababu ya Kutojibiwa**

**Tarehe ya Kuanza:** Februari 1, 2024

Kiungo cha Sera: <https://www.mass.gov/doc/eec-closing-brc-discretionary-review-applications-due-to-non-response-policy-documentswahili/download>

### MUHTASARI

Ili kutekeleza kanuni za sasa, EEC imeanzisha sera ifuatayo ili kuhakikisha kuwa waombaji hawabaki katika au kushirikiana na mpango kwa zaidi ya siku 120 bila uamuzi wa mwisho wa Kukagua Rekodi ya Historia (BRC) kutoka kwenye EEC. Waombaji wa BRC walio katika hali ya kusubiri, kusasishwa, ya muda na/au ya masharti ambao hawatajibu ombi la EEC la kutoa maelezo ya ziada ndani ya siku 120, watatolewa uamuzi wa ufaafu wa "Hawafai" kwa sababu ya kushindwa kujibu. Waombaji wa BRC ambao tayari wamewasiliana na mtoa leseni wao au kitengo cha BRC katika juhudzi za kukamilisha ombi lao la BRC wataongezewa muda wa siku 30.

### MATUMIZI

Sera hii inatumika katika majukumu yote kwa mipango yote yenye leseni na/au iliyofadhiliwa.

### SASISHO MUHIMU

- Kuanzia Februari 1, 2024, waombaji wote wa BRC ambao wamebakia katika hali ya kusubiri, kusasishwa, ya muda na/au ya masharti kwa muda zaidi ya siku 120 na hawajajibu ombi la EEC la kutoa maelezo ya ziada ya, watatolewa uamuzi wa ufaafu kuwa "Hawafai" kwa sababu ya kushindwa kujibu.
- Waombaji ambao tayari wamewasiliana na mtoa leseni wao au kitengo cha BRC katika juhudzi za kukamilisha ombi lao la BRC watapewa siku 30 za kalenda zaidi ya muda wa makataa wa siku 120 ili kukamilisha mchakato wa ukaguzi wa hiari wa BRC. Iwapo, baada ya nyongeza ya siku 30, mwombaji bado hajawasilisha maelezo yote yaliyoombwa, atatolewa uamuzi wa ufaafu kuwa "Hafai."
- Waombaji wote walitolewa uamuzi wa ufaafu kuwa "Hawafai" kwa sababu ya kushindwa kujibu hawataidhinishwa tena kufanya kazi au kushirikiana na mpango ulioidhinishwa na/au unaofadhiliwa na EEC na ni lazima waondolewe kwenye mpango huo ndani ya muda wa siku 14.
- Waombaji wote watapokea barua kuwa Hawafai kupitia barua au barua pepe inayoonyesha haki zozote zinazotumika za kukata rufaa. Mipango itapokea barua kuwa Mwombaji Hafai

kupitia Kituo cha Tovuti ya BRC au Usimamizi wa BRC au, kwa upande wa watoa huduma wa FCC, kupitia barua pepe.

### **RASILIMALI**

[Tafadhali angalia mwongozo wa nyenzo za EEC kuhusu sera hii.](#) Iwapo wewe au wafanyakazi wako mna maswali kuhusu sera hii au mnahitaji usaidizi wa ziada, tafadhali wasiliana na Kituo cha Mawasiliano cha EEC katika 617-988-7841.

### **ISIYOTUMIKA**

Hii ni sera mpya na haichukui nafasi ya sera zozote za sasa za EEC BRC.